



MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR

S.L.P. 3650

**VICTORIA GARDEN
ZANZIBAR**

SIMU: 024 223 2916

MOB: 0774 824242

FAX: 024 223 1461

KATIBU wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said, amesema endapo muhali utaondoshwa kwa watendaji wa Taasisi mbalimbali itasaidia kuondosha vitendo viovu ikiwemo rushwa na dawa za kulevyaa.

Alisema tatizo kubwa liliopo Zanzibar ni muhali, hali ambayo huchangia kwa kiasi kikubwa kuchochea masuala mbalimbali ikiwemo udhalilishaji, rushwa na dawa za kulevyaa hivyo ni vyema jamii na watendaji kuachana na muhali ili kufanikisha malengo ya Serikali.

Mhandisi Zena alisema hayo alipokuwa Mgeni Rasmi katika Chuo cha JKU Kama Wilaya ya Magharibi "A" Unguja katika ufungaji wa mafunzo ya awali ya uchunguzi (BIC) yaliyowashirikisha watumishi 45 kutoka Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA) na Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevyaa Zanzibar.

Alisema wapo baadhi ya watendaji wamekua wakishindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo kwa kuhofia nyadhifa za baadhi ya watu na wengine kuhofia watu wao wa karibu.

"Wapo baadhi ya wafanyakaji wa matukio haya ni wafanyakazi wa Serikali na wengine ni ndugu zao wa karibu hali ambayo husababisha kudhorotesha

mapambano hayo, hivyo ni vyema wanajamii wakashirikiana pamoja ili kutokomeza matukio hayo," alisema.

Alieleza kazi ni moja ya ibada ni vyema kila mtumishi kutekeleza majukumu yake kwa nia moja ili kutegemea ujira kutoka kwa Allah.

"Mafunzo muliyyapata myaendeleze katika utekelezaji wa majukumu yenu kwani wafanyaji wa matukio hayo huwa wamejipanga kupambana na nyinyi," alisema.

Mapema Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Ndugu Seif Shaaban, alisema kuanzishwa kwa ZAECA ni kusaidia kuimarisha uwajibikaji na utendaji ndani ya Serikali. Alisema ili watumishi waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo hakuna budi kupatiwa mafunzo ya mara kwa mara ili yaweze kuwaongoza katika kazi zao za kila siku.

Mkurugenzi Mkuu wa ZAECA, ACP Ahmed Khamis Makarani, nae mapema alisema mafunzo hayo yatawasaidia maofisa hao kuwa na uzalendo, ujasiri na maadili katika kuitumikia Nchi yao juu ya kupambana na vitendo hivyo.

Mkuu wa mafunzo hayo afande Kudura R Hassan alisema mafunzo hayo kwa kiasi kikubwa yatawasaidia vijana hao kwenda kupambana na wahalifu wa matukio hayo ambayo kwa namna moja ama nyengine yanachangia kurudisha nyuma shughuli mbalimbali za kimaendeleo.

Risala ya wahitimu hao iliyosomwa na Ofisa kutoka ZAECA Lela Amour Said, alisema mafunzo hayo yamewasaidia kupata mwanga na msingi mzuri wa kupambana na rushwa na dawa za kulevyahivyo walihidi kwamba wapo tayari kulitumikia Taifa lao wakati wowote.

Mafunzo hayo ya wiki 13 yamewashirikisha Maofisa 45 kutoka ZAECA na Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevyahivyo Zanzibar, ambapo katika hafla hiyo ya ufungaji yalihudhuriwa na Viongozi mbalimbali wa Serikali ya SMZ na SMT, wakiwemo Wakuu wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama.